**HOTUBA YA KUFUNGA MWAKA 2023 ILIYOTOLEWA NA DKT. BONIPHACE NALIJA LUHENDE, WAKILI MKUU WA SERIKALI KATIKA HALFA FUPI YA KUFUNGA MWAKA ILIYOFANYIKA KATIKA OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI, DAR ES SALAAM TAREHE 29 DISEMBA, 2023**

**Wajumbe wa Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali,**

**Watumishi wote wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali,**

**Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,**

**Habari za Mchana,**

**Ndugu Watumishi,**

Napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru, Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na fadhila kwa kutupa nguvu na uwezo wa kufika Mwisho wa Mwaka 2023 tukiwa na Afya njema. Mwaka 2023 ulikuwa na mambo mengi, pamoja na changamoto za hapa na pale lakini kwa uwezo wa Mungu pekee tumefika Mwisho wa Mwaka na tunaimani kwamba tutavuka salama kuona Mwaka ujao wa 2024.

Pia naomba tutumie nafasi hii kumkumbuka Mfanyakazi Mwenzetu, aliyekuwa Mkurugenzi wa Idara ya Mipango Dkt. Abdul Mussa Ally aliyefariki kwa ajali ya gari tarehe mwezi Mei wakati akielekea Jijini Dodoma kikazi. Naomba wote tusimame kwa utulivu kwa dakika moja na tuendelee kumwombea Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema peponi.

**Ndugu Watumishi,**

Pia nitumie nafasi hii kushukuru kila mmoja wenu ambaye alishiriki kwa njia moja au nyingine kufanikisha mafanikio ya Ofisi hii kwa mwaka huu. Naomba

niwakumbushe kwamba kila mmoja wenu ni muhimu na mchango wenu tunauona na kuuthamini. Nawaombea kwa Mwenyezi Mungu awabariki nyinyi na familia zenu na natumaini tutaingia wote salama mwaka ujao ili tuweze kuendelea kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi, weledi na ufasaha zaidi.

Naomba niwahakikishie kwamba mimi, Wakili Mkuu wa Serikali pamoja na menejimenti kwa ujumla tunatambua michango yenu na tumepokea changamoto mbalimbali ambazo tumezifanyia kazi katika mwaka huu. Kutokana na hayo tumeweza kupata mafanikio mbalimbali kama ifuatavyo- ;

**Ndugu Watumishi,**

**Mafanikio hayo yanajumuisha;-**

**1. Uendeshaji wa Mashauri ya Madai na Usuluhishi**

Ofisi imeweza kuiwakilisha vizuri Serikali kwenye Mashauri ya Madai na Usuluhishi na hivyo kuweza kuokoa fedha ambazo zingelipwa kwa wadai. Kwa taarifa tulizokuwa nazo hadi Mwezi wa Tisa, ; Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendesha mashauri 7,392 ambapo kati ya mashauri hayo 7,255 ni ya madai na 137 ni ya usuluhishi ambapo kati ya mashauri hayo 7,350 ni ya ndani ya nchi na 42 ni ya nje ya nchi. Kwa kipindi tajwa hapo juu, Ofisi imemaliza jumla ya mashauri 620 ambapo mashauri 579 yalimalizika kwa njia za kimahakama na mashauri 41 yalimalizika kwa njia ya majadiliano nje ya Mahakama. Pia, Serikali kupitia Ofisi hii imeokoa jumla ya Shilingi Bilioni mia sita na tisa, Milioni mia tatu sitini na nane, laki moja na themanini na nne elfu, mia tatu sabini na nane na nukta thelathini na mbili (609,368,184,378.32) na dola za kimarekani Milioni thelathini na saba

nukta tatu nne (37,341,177) ambazo zingelipwa kwa wadaawa endapo Serikali ingeshindwa kwenye mashauri hayo.

Taarifa ya fedha zilizookolewa na kesi tulizoshinda hadi kufikia Mwezi Disemba, 2021, tutaziweka kwenye Ripoti ya Nusu Mwaka (Bi- annual report) ambayo itakuwa tayari Mwezi Januari, 2022. Naomba tupate nafasi ya kupitia Bi- annual hiyo ili tuwe na ufahamu wa yaliyofanywa na Ofisi kwa kipindi hicho.

**2. Rasilimali watu**

Tunaendelea kuishukuru Ofisi ya Rais Utumishi kwa kuendelea kutuongezea watumishi katika kada mbalimbali ambao kwa umoja wenu mmefanikisha mafanikio ya OWMS kwa mwaka 2023.

**3. Ongezeko la Bajeti**

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Ofisi imeweza kupata ongezeko la Bajeti kutoka kiasi cha **Tshs. bilioni kumi na mbili, milioni mia nane kumi na mbili, laki nane kumi na sita elfu (12,812,816,000) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023** hadi kufikia **bilioni kumi na saba, milioni sabini na tano, laki nane na thelathini elfu (17,075,830,000)** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ambapo ongezeko hilo ni sawa na asilimia **25**.

Kipekee napenda kuchukua fursa hii kumpongeza kwa dhati aliyekuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali ambaye kwa mujibu wa muundo wa Ofisi hii ni Afisa Masuuli, Bi. Sarah Mwaipopo kwa kujenga hoja ambayo imepelekea ongezeko la Bajeti hiyo.

Aidha, niendelea kumpongeza Jaji Mwaipopo kwa kuaminiwa, kuteuliwa na kuapishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania, na Ndg. George Nathaniel Mandepo kuwa Katibu wa Tume ya kurekebisha Sheria Tanzania.

Nawapongeza Watumishi wote kwa ushirikiano na upendo mmaoendelea kumpatia Ndg. Mark Mulwambo katika kipindi hiki anachoendelea kukaimu nafasi na Madaraka ya Naibu Wakili Mkuu wa Serikali hadi hapo mamlaka husika itakapojaza nafasi hii.

Ni imani yangu kuwa watumishi wote wa OWMS mtaendelea kutoa ushirikiano wa kutosha kwa menejimenti ya OWMS na viongozi wote ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu yaliyopangwa kufanyika kwa Mwaka huu wa Fedha kikamilifu ili kama ofisi tuweze kufia malengo tuliyojiwekea kuendana na Mpango Kazi wetu.

## 4. Kufungua Ofisini Mikoani

Ofisi kwa Mwaka huu, inatarajia kufungua Ofisi mpya Mkoani Manyara. Pia tumeendelea kuboresha Ofisi za Mikoani kwa kuongeza watumishi na vitendea kazi.

## 5. Mafunzo kwa Watumishi

Katika Mwaka huu, Ofisi imeendelea kutoa mafunzo kwa watumishi hususani katika sekta ya sheria, mafunzo ambayo yamesaidia kuwajengea uwezo na ujuzi katika sekta ya uwekezaji hasa wa mafuta

na gesi. Aidha, Ofisi imeendelea kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi watumishi wote ambao waliomba kujiendeleza kielimu.

6. **KUBORESHA MIUNDOMBINU YA TEHAMA**

Ofisi imeendelea kuboresha ya TEHAMA, miundombinu ya Maktaba, sambamba na miundombinu ya Kitengo cha Masjala ya Sheria.

Pia tumeendelea kuwagawia watumishi vitendea kazi vya kisasa kwa watumishi ikiwemo Compyuta, laptops, Meza na viti kwa watumishi ili kuboresha utekelezaji wa majukumu ya OWMS.

7. **UJENZI WA OFISI ZA WAKILI MKUU DODOMA**

Tunaendelea na ujenzi wa Ofisi zetu ambazo zitakuwa makao makuu pale katika mji wa Serikali Mtumba, Jijini Dodoma, Ambapo mpaka sasa ujenzi huo umefikia asilimia 47.

**Ndugu Watumishi,**

Tunafahamu kuwa bado zipo changamoto chache ambazo zimekuwa kikwazo katika utekelezaji wa majukumu yetu. Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inaahidi kuendelea kufanyia kazi changamoto zote kwa Mwaka ujao ili kuboresha mazingira ya kazi ba hatimaye tuweze kufikia malengo yote tuliyojiwekea kwa wakati.

**Ndugu Watumishi,**

Natoa rai yangu kwa watumishi wote wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali nchini kuendelea kufanya kazi kwa bidii kwa kufuata misingi sheria, taratibu

na kanuni za utumishi wa umma na kuhakikisha tunatimiza majukumu yetu ya kila siku kwa uadilifu mkubwa. Tukumbuke kuwaheshimu kila moja wetu na kufanya kazi kama timu moja. Nina uhakika kwa kufanya hivyo juhudi zetu zitazaa matunda na matokeo yake yataonekana.

Mwisho, napenda kuwatakiwa Mwaka Mpya mwema, tusiache kusali na kuombeana uzima na afya zenye siha njema. Pia tuendelee kuishi kwa upendo, Amani na mshikamano kwa kudumisha umoja wetu.

**Asanteni sana.**